## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2019 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ifuatayo: 2015, 2016, 2017 na 2018

***Jedwali 10: Matokeo ya KCPE Kiswahili ya 2015 hadi 2019***

| | 2015 | | 2016 | | 2017 | | 2018 | | 2019 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| **Alama ya wastani** | 22.34 | 21.75 | 24.60 | 19.31 | 24.19 | 18.21 | 25.80 | 17.93 | 22.34 | 20.69 |
| **Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi** | 21 | 20 | 24 | 20 | 23 | 20 | 25 | 18 | 21 | 20 |
| **Alama ya juu iliyotuzwa** | 49 | 39 | 48 | 40 | 49 | 40 | 50 | 40 | 48 | 40 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba:

**Katika lugha**:

i) Utendaji wa watahiniwa wa 2019 umedidimia. Hili linadhihirishwa na kushuka kwa alama wastani kutoka **25.80** mwaka 2018 hadi **22.34** mwaka huu.

ii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa mwaka wa 2019 ni **48** ikilinganishwa na **50** ya mwaka wa 2018. Ni watahiniwa **wawili (2)** tu waliopata alama hii.

iii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **21** tofauti na **25** ya mwaka 2018

iv) Alama wastani imeshuka kwa alama **2.66** kutoka kwa kiwango kinachokubalika cha **(25/50).**

v) Alama tenganishi ilikuwa 6.43. Hii ina maana kuwa watahiniwa wengi walipata kati ya alama 15.91 hadi 28.77. Hii ni ishara kuwa maswali yaliwatenda watahiniwa ipasavyo.

**Katika Insha:**

i) Alama ya wastani imeimarika kwa alama **2.76** kutoka **17.93** mwaka wa 2018 hadi **20.69** mwaka huu.

ii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa mwaka 2019 ni **40.** Alama hii iko sawa na alama iliyotuzwa mwaka wa 2018. Mwanafunzi **mmoja (1)** ndiye aliyepata alama hii.


iii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **20** tofauti na **18** ya mwaka 2018. Hii ni alama ya wastani kwa kuwa jumla ya alama zituzwazo katika uandishi wa insha ni **40.**

iv) Alama tenganishi ilikuwa 7.30. Hii inaonyesha kuwa watahiniwa wengi walipata alama kati ya 13.39 hadi 27.99.

v) Alama ya wastani inaashiria kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi wa darasa la nane wamejizatiti kuimudu lugha ya Kiswahili haswa katika kujieleza kwa ufasaha na kwa ubunifu. Tunawapongeza walimu wa Kiswahili kwa juhudi zao za kuwaelekeza wanafunzi kupata umilisi ufaao wa kimsingi

unaohimizwa katika ujifunzaji wa lugha hii. Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi alama za sehemu za Lugha na Insha zilivyojitawanya.

**Mchoro 4**





## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

### 4.1.1 Uchanganuzi wa maswali maalum

Mchoro ufuatao unaonyesha asilimia ya watahiniwa ambao walipata jibu sahihi katika kila swali:

**Mchoro 5**




### 4.1.2 Uchanganuzi wa maswali yaliyowatatiza watahiniwa

Katika mwaka wa 2019 yapo maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa. Watahiniwa waliopata majibu sahihi kwa maswali haya walikuwa chini ya asilimia thelathini **(30%).** Maswali yafuatayo ndiyo yaliwatatiza watahiniwa zaidi: Swali la **13, 19, 22,40, 41** na **48**.

*Jedwali 11: Maswali ambayo yaliwatatiza zaidi watahiniwa*

| Maswali | 13 | 19 | 22 | 40 | 41 | 48 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sahihi | 24.36 | 16.11 | 9.97 | 11.71 | 15.58 | 20.03 |
| Asilimia ya wastani ya maswali yale mengine | 24.73 | 25.80 | 21.70 | 25.05 | 26.61 | 21.30 |

### 4.1.3.1 Ruwaza za majibu

**Swali la 13**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi **1** mpaka **15**. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo **zaidi** kati ya yale uliyopewa.*

__**8**__ na Kani katika kidato cha kwanza. Kani alikuwa____9___ wanafunzi bora __**10**__ kuona. Hakukata tamaa hata __**11**__ masomoni. Kani alikuwa rafiki wa dhati. Alinisaidia __**12**__ aina za maneno kama vile __**13**__ ambayo ni vivumishi. Pia alinifunza kutenga silabi katika maneno mbalimbali. Kwa mfano, neno 'nywesheana' lina silabi__ **14** __. Aidha, aliniambia kwamba umoja wa sentensi, 'Mazulia hayo yao yalifumwa na washonaji wale,' ni: __**15**__ .

**8**. A. Nimekutana B. Ningekutana C. Nilikutana D. Nikakutana
**9**. A. miongoni mwa B. mkabala mwa C. baadhi ya D. mithili ya
**10**. A. niliyewahi B. niliowahi C. aliowahi D. aliyewahi
**11**. A. alipoharibikiwa B. alipoharibiwa C. alipoharibikia D. alipoharibia
**12**. A. kumfunza B. kujifunza C. kutufunza D. kuwafunza

**13**. A. sana, nene, fupi, kama
B. nyingine, ajabu, mwenyewe, kisha
C. kijanja, tano, langu, leo
D. kadha, yule, chungu, lote

**14**. A. 5 B. 6 C. 4 D. 3

**15**. A. Zulia hilo lao lilifumwa na washonaji wale
B. Mazulia hayo yao yalifumwa na mshonaji yule
C. Zulia hilo lake lilifumwa na mshonaji yule
D. Mazulia hayo yake yalifumwa na washonaji wale

**Matokeo ya swali la 13**

| Majibu | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 35.94 | 27.19 | 11.70 | 24.36 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 21.58 | 21.42 | 21.27 | 21.02 |

Swali hili ni la kiuchanganuzi lililolenga ufahamu wa mwanafunzi wa kubaini aina za maneno. Mtahiniwa alihitajika kuchagua kundi la maneno ambayo ni vivumishi peke yake. Kivumishi ni neno linatoa sifa kuhusu nomino au kiwakilishi chake. Wengi wa watahiniwa walichagua jawabu **A** pasi na kufahamu kuwa *sana* ni kielezi (kwa kuzidi). Aidha neno *sana* laweza kuwa kitenzi elekezi likiwa na maana ya kutengeneza vitu au mapambo kutokana na madini; fua. Kwa upande mwingine neno

*kama* linaweza kuwa ni kiunganishi kwa maana ya ikiwa au endapo. Isitoshe neno *kama* humaanisha kuliko. *Kama* pia laweza kutumiwa kama kielezi kwa maana ya kiasi cha (kwa kukisia tu). Kwa mfano kulikuwa na wanafunzi *kama* mia tano hivi alipofika kwenye sherehe. Pia *kama* ni kitenzi elekezi kwa maana ya kutoa maziwa kwenye kiwele cha mnyama (kamua). Maana nyingine ni finya kwa nguvu. Asilimia nyingine kubwa walichagua **B** pasi na kufahamu kuwa *ajabu* ni kielezi na vilevile *kisha* ni kielezi cha wakati.

**Swali la 19**

**19.** Chagua jibu lenye kivumishi kilichoundwa kutokana na kitenzi.

A. ita – mwito
B. sahau – sahaulifu
C. agiza – maagizo
D. vumilia – uvumilivu

**Matokeo ya swali la 19**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 15.15 | 16.11 | 17.45 | 50.55 |
| **Alama ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.72 | 25.80 | 20.75 | 21.84 |

Hili lilikuwa swali la kiuchanganuzi ambalo lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kubainisha jibu lenye **kivumishi** kilichoundwa kutokana na kitenzi. Hapa mtahiniwa sharti afahamu fika kivumishi na kitenzi ni kipi katika lugha ya Kiswahili ndipo aweze kupata jibu sahihi. Watahiniwa wengi walichagua jawabu **D.** Uvumilivu ni nomino *dhahania* bali si kivumishi.

**Swali 20**

**20.** Ni sentensi ipi inayoonyesha kusudi la tendo?

A. Suna aliingia zizini akawafungulia ng'ombe, akaelekea malishoni.
B. Malika alituambia twende tukavue samaki.
C. Wafanyakazi walifanya bidii wakamaliza kazi hiyo.
D. Wageni watakuja watakapokamilisha shughuli.

**Matokeo ya swali la 20**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 38.19 | 16.64 | 23.96 | 20.40 |
| **Alama ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.36 | 22.64 | 21.52 | 22.71 |

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuchunguza aina za sentensi alizopewa ili kubaini ni gani inayoonyesha *kusudi la tendo.* Jawabu sahihi linadhihirisha wazi sababu ya Malika kuwaomba waende. Lengo la kwenda ni *kuvua samaki.* Jibu la **A** linaonyesha mfuatano wa vitendo unaowakilishwa na kiambisha **ka**. Jibu la **C** ni taarifa na lile la **D** linaonyesha masharti. Kuja kwa wageni kunategemea kukamilisha shughuli waliyokuwa nayo.

**Swali la 22**

22. Chagua jibu lenye viambishi vya neno: funguliana.

A. fu-a-na
B. li-an-a
C. fu-an-a
D. li-a-na

**Matokeo ya swali la 22**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 27.43 | 9.97 | 9.67 | 52.14 |
| Alama ya wastani ya maswali yale mengine | 20.97 | 21.70 | 20.13 | 23.47 |

Swali hili ni la kiuchanganuzi. Mtahiniwa alihitajika kuwa na uelewa wa viambishi. Kiambishi ni silabi inayopachikwa kabla au baada ya mzizi wa neno. Mzizi ukiwa ni ile sehemu ya neno ambayo haibadiliki na hubeba maana ya kimsingi ya neno hilo. Neno walilopewa **funguliana** halina viambishi awali bali lina viambishi tamati; **li-an-a**

**Swali la 40**

40. Wanachokiita 'ukali wa wazazi' ina maana kwamba mwandishi:

A. anakana kuwa wazazi ni wakali;
B. anahofia kuwa wazazi ni wakali;
C. anadai kuwa wazazi ni wakali;
D. ameamini kuwa wazazi ni wakali.

**Matokeo ya swali la 40**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 12.41 | 28.93 | 29.65 | 28.27 |
| Alama ya wastani ya maswali yale mengine | 25.05 | 21.67 | 23.88 | 19.99 |

Swali hili ni lilimhitaji mtahiniwa kuchunguza yaliyomo kwa makini ili kutambua maana ya kauli ***ukali wa wazazi*** kwa kuegemea mtazamo wa mwandishi. Wanachokiita *ukali wa wazazi* kwake mwandishi ana maoni tofauti. Mwandishi anakana wazo hilo kuwa wazazi ni wakali. Watahiniwa wengi hawakumakinika bali walichukulia kuwa swali linawalenga vijana hivyo wakachagua jawabu **C**. Ni muhimu mtahiniwa alisome swali mara kadhaa ili kung'amua kinachotahiniwa.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* **41** *mpaka* **50**.

Kisa kuhusu shughuli ya wanyama kuchimba kisima husimuliwa kwa msisimko mkubwa katika jamii nyingi. Inasemekana kuwa wanyama, wakiongozwa na mfalme wao Simba, walikuwa wakiishi kwa amani na ushirikiano. Siku hizo, shida za mnyama mmoja zilikuwa za wanyama wote. Wale waliokuwa maskini walisaidiwa kwa chakula. Wale ambao walikuwa wenye tamaa kama vile Fisi hawakusita kuonywa dhidi ya kutamani vya wengine. Wale waliokuwa watepetevu na wenye hila kama Sungura nao walishauriwa kuchanika kwenye mpini. Alimradi kila mnyama alijifunga masombo kujenga jamii yenye utu na ustawi.

Hali iliendelea kuwa shwari, jamii ya wanyama ikijitosheleza kwa chakula msimu baada ya mwingine hadi mvua ilipogoma kunyesha. Ukame mkubwa ulijiri; ardhi na mimea ikakauka, wanyama na makinda wao wakawa katika hatari ya kupukutishwa na njaa pamoja na jua lililowaka kama tanuri. Baada ya kuwaza na kuwazua, Simba aliitisha mkutano wa wanyama ili washauriane kuhusu namna ya kukabiliana na hali ambayo ilikuwa tayari kukiangamiza kizazi cha wanyama.

Mkutano ulianza saa tatu asubuhi. Kila mnyama alijihimu kufika mapema. Kobe na Sungura ndio waliokuja wamechelewa kama desturi. Basi baada ya kusafisha koo, Simba alisema, "Ndugu zangu, nimewaita hapa ili kujadiliana kuhusu jinsi tunavyoweza kukabiliana na hali ya ukame na njaa iliyotukumba. Ingawa maghala yetu bado yana nafaka, hali hii ya ukame ikiendelea, mifugo wetu watakufa."

Kila mnyama alitoa maoni yake. Hatimaye waliafikiana kwamba wachimbe kisima kwa zamu ili wapate maji ya kunywa na kunyunyizia mimea. Simba alimwomba Nyumbu aandike ratiba ya jinsi kazi itakavyoendelea. Alisema pia kwamba ikiwa katika siku ya kwanza maji yakatakuwa yamepatikana, basi atakayekuwa ameyapata atatunukiwa zawadi. Kauli hii ilimfanya kila mnyama kutaka kuwa wa kwanza kuchimba. Mabishano makali yalitokea hadi pale Simba mwenyewe alipoamua kwamba ndiye atakayekuwa wa kwanza, kisha afuate Ndovu, Twiga Kifaru... na mwishowe Sungura. Alipotaja jina la Sungura, wanyama, hasa wale wakubwa, walicheka, wakishangaa vipi Sungura na umbo lake dogo atakavyoweza kuutifua udongo kupata maji.

Zamu ya Simba ilifika, akaelekea kulikokuwa kumetengwa kuchimbwa kisima. Alitifua udongo kwa maringo na nguvu zake zote lakini kilichotokea ni vumbi tu. Aliondoka huku amejiinamia na kusimama kando. Ndovu alijua kwamba unene wake utamwezesha kutekeleza yale yaliyomshinda Simba. Alijaribu mara ya kwanza, ya pili, ya tatu... matokeo yakawa yale yale ya Simba. Ndovu alishusha pumzi kubwa, akatikisa kichwa na kuondoka, akaketi chini ya mti na **kushika tama**. Twiga, Kifaru na Duma walifuata lakini matokeo hayakuwa tofauti na ya wenzao; wote waliigonga ardhi kwa vichwa vyao, wakasalimiwa na vumbi tu.

Sasa ilikuwa zamu ya Sungura. Wanyama walimtazama kwa bezo huku wakijua kuwa Sungura hataweza lolote. Sungura aliinama kando ya mti mmoja mkubwa, akatoa mtaimbo na kuuchomeka kwenye kichwa chake. Wanyama wengine walipomwona **walicheka hadi mbavu zikavunjika**. Sungura aliitalii ardhi kwa makini kabla hajaanza kuichimba kwa mtaimbo uliokuwa kichwani mwake. Baada ya dakika kumi za kuchimba, milizamu ya maji ilijitokeza ghafla na kuwalovya wanyama wote. Ardhi sasa ilijaa unyevu, mimea ikaanza kuchipuka mara moja. Wanyama walimtazama Sungura kwa mshangao mkuu. Hakuna aliyenena lolote, wote waliinamisha nyuso chini. Sungura alichukua kipaza sauti na kusema kwa fahari kuu, **"Ndugu zangu, wakati wa vita wale wanaonusurika si walio na silaha kali bali wale wanaojua namna na wakati wa kuzitumia silaha hizo".**

**Swali la 41**

41. Kulingana na aya ya kwanza, wanyama:
   A. waliishi kwa amani kutokana na uongozi wa Simba;
   B. walijali masilahi ya wale waliokuwa wanyonge;
   C. walishangazwa na wanyama waliotamani vitu;
   D. walichangamkia hadithi zilizohusu kuboresha hali zao.

**Matokeo ya swali la 41**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 76.18 | 17.84 | 1.97 | 3.32 |
| **Alama ya wastani ya maswali yale mengine** | 21.52 | 26.61 | 16.17 | 19.82 |

Swali hili ni ni la ufahamu. Mtahiniwa alifaa kusoma kwa kina ili kumaizi yaliyomo katika aya ya kwanza. Wazo kuu katika aya hii ni kujali maslahi ya wenzao haswa waliokuwa wanyonge. Zingatia ujumbe kutoka sentensi ya tatu hadi ya mwisho katika aya hiyo ya kwanza. Asilimia kubwa iliegemea katika uongozi wa Simba ambao hujatiliwa mkazo katika aya hii.

**Swali la 48**

**48. "Ndugu zangu, wakati wa vita wale wanaonusurika si walio na silaha kali bali wale wanaojua namna na wakati wa kutumia silaha hizo".**

Chagua methali inayoweza kujumuisha ujumbe wa kauli hii.

A. Makaa hayaoki nyama.
B. Kisu kibutu hakichinji kuku.
C. Jina la sifa huletwa na matendo.
D. Chombo imara hustahimili mawimbi makali.

**Matokeo ya swali la 48**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 5.81 | 20.03 | 39.88 | 33.52 |
| **Alama ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.15 | 21.30 | 22.33 | 20.24 |

Swali hili lililenga kitengo cha usanisi. Hapa mtahiniwa anahitajika kuleta mawazo pamoja kuhusu kile alichokisoma ili abainishe methali itakayofaa maelezo yaliyotolewa. Kulingana na kauli iliyoko hapo juu, wakati wa vita wale wanaonusurika si walio na silaha kali bali wale wanaojua namna na wakati wa kutumia silaha hizo. Hii ina maana kuwa lazima pawepo na mikakati ya kutenda kazi ili kufanikiwa. Hivyo basi kisu kibutu hakichinji kuku ina maana lazima kitiwe makali ili kitekeleze kazi yake.

**4.1.3.2 Hitimisho**

Kutokana na uchanganuzi wa mtihani wa mwaka 2019, ni dhahiri kwamba utendaji wa wanafunzi katika karatasi ya Lugha utaimarika iwapo wanafunzi watajikakamua kufahamu kwa uketo vipashio vya kimsingi vya lugha kama vile maneno na aina zake. Vipengele vyote vya kisarufi vinapaswa kusisitizwa. Aidha kumakinika katika uelewa wa swali kabla ya kulijibu kunahitajika. Kadhalika, asilimia ya watahiniwa wanaomudu maswali ya ufahamu inaendelea kuongezeka. Asilimia kubwa haikutatizika na maswali ya ufahamu kama ambavyo ilikuwa kawaida katika mitihani ya miaka ya awali. Hata hivyo, bado pana haja ya wanafunzi kuelekezwa kujifunza mikakati bora ya kukabiliana na maswali ya ufahamu.

Hali kadhalika, imebainika kwamba watahiniwa bado wanafanya vyema zaidi katika Ufahamu wa kibunilizi ikilinganishwa na utendaji katika ufahamu wa kimaelezo. Ni muhimu walimu kuwelekeza wanafunzi kuibua mikakati ya kukabiliana na aina zote mbili za Ufahamu. Pia, wanafunzi wanastahili kuhimizwa kusoma kwa mapana ili kujistawisha zaidi katika Ufahamu wa Kusoma.

## 4.2 SEHEMU YA PILI – INSHA

Katika mwaka wa **2019 mada** ya insha ilikuwa:

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo*:
**Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.**

Hii ni insha huria ya kusimulia na lazima mtahiniwa amalizie kwa maneno aliyopewa.

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kubuni utungo ambao unaonyesha kuwepo kwa mambo yasiyo mazuri yanayoleta maafa, majanga, shida n.k. Aidha utungo huu ulipaswa kuonyesha matendo ya vishawishi vilivyomvutia mwandishi au mhusika pasipo yeye kuwazia.

Vipengele vifuatavyo vya insha ya aina hii vizingatiwe:

a) **Maudhui/yaliyomo**
Hapa mtahiniwa alihitajika kutunga kisa kinachoonyesha vishawishi mbalimbali kama vile:

a) Mchezo wa Kamari unaomletea athari ya kutumia karo ya shule, kumwachisha shule, kufungwa jela n.k.
b) Biashara haramu inayoweza kuleta hali ya utekaji nyara, mauaji yanayosababisha kufungwa jela, ulanguzi wa dawa za kulevya unaomfanya afungwe jela n.k.
c) Kuhamia nchi nyingine / mijini kutokana na ushawishi wa marafiki. Athari zake ni mateso au dhuluma, vifo, kufungwa jela kwa kukosa hati za usafiri.
d) Ugaidi kama vile kujiunga na vikundi haramu kama vile Mungiki na Al-shabab kisha kuingia katika vitendo haramu ambapo pana uwezekano wa mtu kufungwa gerezani, kuuawa au kutengwa na jamii.
e) Tamaduni potofu kama vile: ngoma za matangani, ukeketaji na ndoa za watoto. Athari zake ni kupata maradhi kwa wale wanaoshiriki mapenzi. Kupata mimba za mapema, vifo na hata maradhi kutokana na ukeketaji, kuacha shule na ndoa za mapema hususan kwa vijana walio chini ya umri wa miaka kumi na minane.
f) Wizi ambao athari zake huwa vifo, kufungwa jela na hata jamii yote kuathirika.
g) Uraibu kutokana na mitandao ya kijamii ambao husababisha utovu wa maadili.
h) Imani potovu inayomfanya mtu kushawishiwa kuhama kutoka kwa imani yake inayokubalika na kuingia katika imani mbaya au ibada potovu ambapo kwa athari zake huwa ni kudorora kwa maadili au upungufu wa maadili na hata vifo.
i) Kushawishika kushiriki dawa za kulevya kama vile pombe, mihadarati na kadhalika ambavyo kushiriki huku huathiri afya, huchangia vifo, kufungwa jela, maradhi, utovu wa usalama, kusambaratika kwa familia.

Ruwaza zifuatazo zilliweza kujitokeza katika tungo za watahiniwa:

**Tanbihi**

i) Mtahiniwa alipaswa kuandika kuhusu vishawishi mbalimbali kutoka kwa marafiki wabaya ambavyo vilileta athari hasi. Mtahiniwa hivyo basi hakubanwa kwa mifano iliyotolewa hapo juu mradi alijieleza vyema kulingana na swali.

ii) Insha ya mtahiniwa ilifaa iangazie mambo yafuatayo:
- Mhusika
- Marafiki walitoa ushawishi
- Vishawishi au ushawishi
- Madhara yaliyotokana na ushawishi.

b) **Uhusika:**

Katika utungo huu:

i) Mwandishi angekuwa mhusika mkuu.

ii) Mwandishi angeweza kusimulia kisa/mambo yaliyoathiri wahusika wengine au mhusika mwingine.

iii) Marafiki waliotoa ushawishi.

**Tanbihi**

- Paonekane mwathiriwa na anayeathiri/wanaoathiri (wahusika wawe wa aina mbili)
- Huenda kukatokea mhusika mwingine ambaye mwandishi alishuhudia matendo yake.
- Dhana ya ushawishi kutoka kwa marafiki ijitokeze.
- Iwapo mtahiniwa ametumia wanyama kama wahusika basi ilibidi aonyeshe funzo alilopata kutoka kwa kisa cha wanyama hao.

**b) Muundo na mtindo**

**Muundo**

Kimsingi hii ilikuwa insha ya kimasimulizi. Mtahiniwa alihitajika kusanisi kisa ambacho kinaonyesha namna ambavyo alishawishika na matokeo hasi ya ushawishi huo.

Yafuatayo yalitarajiwa kubainika:

**i)** **Mwanzo** – Kiini cha masimulizi kibainike

**ii)** **Mwili** –Hapa ndipo mtahiniwa anapoikuza mada kwa kudhihirisha alivyoshawishiwa na athari za ushawishi huo.

**iii)** **Hitimisho-** Hapa ndipo mtahiniwa anapohitimisha utungo kwa maneno aliyopewa. Aonyeshe hali ya kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

**Mtindo**

i) Mtindo wa kimasimulizi udhihirike

ii) Uteuzi mwafaka wa vipengele vya lugha kama vile methali uzingatiwe.

iii) Kaida za kisarufi zizingatiwe.

iv) Maendelezo mwafaka ya maneno yazingatiwe.

v) Insha iandikwe kwa hati nadhifu inayosomeka.

vi) Aya zibainike vilivyo.

### 4.2.1 Vigezo vya kutathminia

Yafuatayo ni maelezo yanayoonyesha jinsi watahiniwa wanavyotengwa katika viwango/vitengo vinne maalum na mambo ambayo yanazingatiwa ili kumtuza mtahiniwa kiasi fulani cha alama katika vitengo hivi vinne. Vifuatavyo ndivyo vitengo (makundi) vya alama:

(i) 01 – 10
(ii) 11 – 20
(iii) 21 – 30
(iv) 31 – 40

### 4.2.2 Ugavi wa alama za insha

Mpangilio wa alama zituzwazo kwenye kila kipengele ni kama ufuatao:

i. Maudhui - 20
ii. Msamiati na matumizi yake - 12
iii. Mtindo na muundo wa insha - 05
iv. Mtiririko na mshikamano - 03

**Jumla ya alama- 40**

### 4.2.3 Kundi la kwanza (alama 01 – 10)

Watahiniwa katika kitengo hiki hawamudu kujieleza katika Kiswahili. Watahiniwa wanaopata alama **01-06** hasa huwa na mtindo hafifu sana wa kujieleza. Insha zao hukosa muwala na muumano wa mawazo. Baadhi hujieleza kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zao za mama. Wengine hutumia maneno yasiyoeleweka kabisa. Msamiati hutumiwa kiholela bila uwiano wowote, ama na misamiati jirani, au na mada husika. Udhaifu wao wa kimawasiliano huwakosesha kuikuza mada au kuyafafanua kwa kina maudhui ya swali walilopewa.

Watahiniwa wanaotuzwa alama **07-09** hudiriki kujieleza kwa Kiswahili, japo kwa mtindo hafifu. Insha zao huwa na mategu mengi ya sarufi na hijai ambayo huufifilisha usimulizi/kujieleza kwao. Hawa pia huwa wamepotoka au kupungukiwa kimaudhui (kulingana mada) na wengi huhamisha sheria za lugha zao za mama hadi Kiswahili (huwa na athari nyingi za lugha ya mama).

**Mtungo wa kwanza**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Kadika siku moja katika settemu ya lindi in pallal in muvuriy ya watu wakubwa na wadoga yeye wajiwezi kimalsha yao ya leo na kesha na wa kuje na kina mama na kina baba wapewe chakula ya kupika Nyumbain yao na kufura kiwatu wa Nyumba moja walioisi pamoja kihafurika ya ichi yali kenya ya kihafurica. bahada ya siku mbili walikuwantabiya muzuriy ya kistarbu ya kihafurica in muzuriy kujuwan ki marafiki wa leo na piy kesha na hurafiki yetu uliendele ya to kifurahi ya katika nyumba moja ya watu wegi sana katika Nyumba moja.

Siku moja katika Nyumba ya buwan kerry Hahifeng neza ziwiry Nyumba yake halifurahifa sana kimoja wa unguwan siku moja kerry Halipatan na rafiki yake alimusalimiy habari yako. Habari yangu ni zuriy sana katika

maisha yako in muzuriy sana yaki maisha
ya kesha piy keshokutuwa maisha
yangu in muzuriy sana hadi intasahidi
yana na wenzangu.

Katika maisha in kusahadihan
weye wajiwe zi kujisahaldiya kimaisha
ya kesho na piy watoto wengi ne weye
wa jisahidiya na kusahidihan kimaisha
ya Leo na kesho na kusema Hasante
sana kwa kunisahidiya na piy kumu
shukuru sana kimaisha yako na piy
ya mutu minginene kimaisha yao nashukuru.

siku moja katika settemu
za mubatta ya ije ya kenya in kutembe
leya watu wengi nene na piy kumusahidiya
Ije ya kenya kuhinu wa bendera ya
kenya in pattali ya watu hupumuzika
na kuongele ya zito zizoriy sana katika
settemu zingine za kenya in mahali hil
pahazuriy pahati watu husikiliza
katika maneno mazuriy yeye
watu hufurahi ya waki sikiya katika
mahali pahazuri pahali watu wana
stahi hil kuka wa kizu gumuza manena
ya watu wakubuwa.

Mtahiniwa huyu anajaribu kujieleza kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, lugha yake ni hafifu mno. Utungo wake umejaa mategu ya kisarufi na kihijai. Mtahiniwa huyu hajailewa mada wala kuiandikia. Amepangilia mawazo yake kiaya na hivyo alituzwa alama za mtindo na muundo. Aidha alituzwa alama za msamiati alioutumia licha ya kuwa ni wa kiwango hafifu.

Alama iliyotuzwa: **04**

**Mtungo wa Pili**

## SIKU AMBAYO SITA WAHI SAHAU

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Ninakumbuka vizuri ilikuwa siku ya Jumaa ambapo nilirauka lau lau ili nijitayarishe ilikujitayarisha kwenda shuleni, Nikajitoza bafuni nakutoka nikiwa safi kama maji ya bahari. Nilirudi chumbani changu cha kulala na kuvalia sare zangu za shule, kisha nikatoka. Nilienda kwenye kituo cha basi na kungojea matwana ile.

Muda si mudo matwana ikawasili, Niliuabiri ili nisiweze kuchelewa shuleni. LO! Kumbe dereva wa matwana hiyo alikuwa mlevi. Alikuwa anaendesha matwana hiyo kwa kasi ya duma. Lakini pia hiyo ilikuwa faida kwangu. Niliwasili shuleni kabla ya mwalimu wangu kuwasili.

Nilipoingia darasani, niliwakuta wanagenzi wenzangu wanapiga kelele darasani, wengine walikuwa wanaruka juu ya dawati za wengene. Nilipowaambia wanyamaze wakaanza kunitusi na kusema kuwa mimi ninajifanya kiranja, punde si punde mwalimu

wetu akaingia.

Darasa nzima ilinyamaza kama maji ya mtungi. Mwalimu wetu akaniambia niende niketi. Niliendo kwa utaratibu moja kwa moja hadi kwenye dawati langu. Lakini nilipoketi, niliwasikia kikundi ya vijana nyuma yangu waki panga vile wange toroka shuleni baada ya mwalimu kutoka.

Kisha mmoja wao akaja na kuniambia niende na wao, kwa kuwa walikuwa marafiki zangu nilikubali na kuenda nao. Baada ya mwalimu kutoka hivi nasi tukatoka. Lakini tulipotaka nje ya shule hivi tukakutana na mwalimu mkuu. Hakika nilikuwa kuganduo kwamba ni muhimu kuwazia hatari yde ya mambo marafiki wanatenda.

Mtahiniwa huyu hajakuza mada ipasavyo. Amedokeza tu maudhui katika aya ya mwisho. Matumizi ya maneno katika sentensi yameathiriwa sana na ubovu wa sarufi, hijai, uakifishaji na makosa ya njeo.

Hata hivyo, Mgalla muuwe na haki umpe, mtahiniwa huyu ametumia mtindo hafifu wa kusimulia. Muundo wa insha yake umebainika kwa kiasi fulani haswa katika umbo la insha ya aina hii. Hati yake inasomeka, aya zipo lakini hazijitoshelezi.

Alama iliyotuzwa: **09**

**Kundi la Pili (alama 11 – 20)**

Kundi hili huwa na watahiniwa ambao wanaimudu lugha kiasi. Wanaweza kujieleza au kusimulia kwa sentensi au kauli zinazoleta maana. Wale wanaotuzwa alama **11 - 15** huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, na insha zao hukosa mtiririko mzuri wa mawazo. Wengi huwa bado na athari za lugha za kwanza/lugha za mama.

Wanaotuzwa alama **16 - 20** huwa wameimudu mada kiasi na mtindo wao wa uwasilishaji huwa bora zaidi, ingawa bado huwa chini ya wastani. Wanaweza kutumia msamiati wa kuvutia hapa na pale japo kwa kawaida wengi huutumia msamiati wenyewe vibaya. Insha zao kwa kawaida hutosheleza urefu.

**Mtungo wa Tatu**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Tulikuwa tuna paka katika kijiji ya matopeni. kijiji hicho, kina watu mbali mbali ni pali uwezi jua na ni wa kaye mwamini, Ni kona marafiki ambao wa na paka kama watoto wamtani mtoni matopeni kum kuwa na ufisadi mwingi hata kwaserikali matopeni kila kitu ili kuwa inaenda kinyume na sheria abaza zinafa kutumika.

Kanora wenye tama kuiba. Ni likuwa na marafiki kama hao tuli kuwa tuna fanya wizi tukiiba tulikuwa tunaenda kuuza kile ambacho tuli cho iba. Nilika kijana mzuri ambye a naenda kani sani, lakini nilipo kuwa marafiki na kijana wa mtaani nili kuwa niki tembea naye kwanzia hasubuhi hadi usiku

Rafiki huyo alinipeleka wamarafiki zake wale ambo wana tumia bangi, sigara, madawa zakulevya, rafiki yangu alikuwa ana nipatia bangi nijari, ni tumia mada wa hizo, hadi tuka choka nika zikora.

Nilikuwa ni kienda kwangyumba mzazi wangu: alikuwa hadi analia, akiniambia ni wache kufuta madawa hizo nilikuwa hadi silalikwa nyumba nacoda kula la pabali tulikuwa tuki fanyia mambo zetu.

Nilikuwa nashinda nikiwamlevi sana, madawa hizo zilikuwa zinafanya nina sahau kama kitakitu ambayo nilikuwa nina juwa hata mlango yakanisa Sikuwa na juwa inatiwanga wapi hata maapisi kuwa natumbua

Siku moja hapo ndipo nilikuwa nimegunduwa kuwa mamazazingu ana teseka sana kwangu. Nilimwambia: mama pole sana nahapo ndipo nilise ma sitatumia madawa hizo tena nika okoka tena.

Mtahiniwa huyu licha ya kuwa na changamoto si haba za msamiati na matumizi yake, amedokeza uelewa wa mada lengwa. Yeye na marafiki wake walikuwa na tabia ya kuiba na vilevile kushiriki dawa za kulevya. Matukio yaliyomo katika utungo huu yanaakisi kwa kiwango fulani taswira tarajiwa. Yaani utungo huu una wahusika ambao ni marafiki waliomshawishi msimulizi. Makosa ya kisarufi na hijai ni mengi mno. Hata hivyo vipengele vya mtindo na muundo vinadhihirika. Kwa mfano hati inasomeka na vilevile aya zipo.

Alama iliyotuzwa: **13**

**Mtungo wa Nne**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Katika kijiji cha makazi palishi na msichana mója aliyetwa Lulu. Lulu alikuwa msichana mrembo kama tausi, kila mtu alimpenda kwa sababu alikuwa msichana mpole sana. Siku moja Lulu alipokuwa akielekeya nyumbani alikutana na marafiki waliyokuwa wakisoma nao katika shule ya chekecheya. Marafiki hao walikuwa wakimlazimisha Lulu kuzitumia dawa za kulevya, lakini Lulu halikata katakata, kwa sababu halijuwa madhara ya dawa hizo na kuenda nyumbani.

Marafiki zake walizidi kumwambia hajaribu kutumia hili kupunguza mawazo zake. Lulu alijaribu mara moja na hakajuwa jinzi ya kupunguza mawazo zake ni kutumia dawa za kulevya. Mama yake alishikuwa na wasiwasi kwa sababu hakujuwa hafanye nini wala hatende nini kwa sababu Lulu hakutaka kufuata maelezo aliyokuwa hakipewa na mama yake.

Badaa ya wiki moja Lulu alienda kujiunga na marafiki wapotevu. Marafiki zake walimtafutia nyumba ya kuishi yeye na marafiki zake. Walitumia dawa hiza hadi zikawaribu viyungo vya mwili kama vile ubongo. Marafiki zake Lulu walimtafutia kijana mtamashati na kumleteya Lulu. Kijana huyo alikuwa mtamashati lakini alikuwa na UKIMWI lakili hakuna haliyejua.

Siku moja kijana huyo halitaka kufunga ndoa na Lulu. Lulu hakukata kwa sababu kijana huyo alikuwa na pesa yenye alisema kaotaka kitu angempa. Badaa ya siku chache kijana huyo na Lulu walifunga ndoa wakiwa na furaha riboriba kama aliyejifunguwa radha salama salmini, lakini hawakuacha kutumia dawa za kulevya kwa sababu wote wawili walikuwa wakizitumia.

Siku moja Lulu aliamuwa kuenda hospitalini kupimwa na daktari kwa sababu alidhani kwamba yeye ni mjamzito. Daktari alimpeleka kwa chumba moja na kumpima na kumwambia kwamba yeye ni mjamzito na pia ana UKIMWI. Lulu alikuwa na hasira kwa sababu alijuwa kuwamba mume wake alikuwa na UKIMWI.

Lulu alimuliza mume wake kwa nini hajawahi kumueleza kama yuko na UKIMWI. Mume wake alimwambia kwamba marafiki zake walimwambia asimweleze ndiyo kwa sababu hakutaka mambo haya kuwake. Hakika nilikuwa kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafi wanatenda.

Mtahiniwa huyu amebainisha kuimarika zaidi. Ameielewa mada na kuikuza vyema zaidi akilinganishwa na watahiniwa wa awali. Ametumia tamathali chache za usemi kwa mfano, **nahau**- kufunga ndoa, **Tashbihi** – mrembo kama tausi.

Hata hivyo, utungo wake una makosa mengi ya kihijai, kisarufi na kimsamiati kama vile:

a) Tahajia, kwa mfano, **aliyetwa badala ya aliyeitwa, akielekeya badala ya akielekea, hajaribu badala ya ajaribu, badaa badala ya baada, jinzi badala ya jinsi n.k.**
b) Kijana mtamashati badala ya kijana mtanashati.
c) Muundo usiofaa ambao unasababisha upatanisho usiofaa wa kisarufi. Kwa mfano, **msichana moja badala ya msichana mmoja.**

Utungo wa mtahiniwa huyu ni mkavu na hauna mvuto kwa kuwa hajamakinika katika kutumia tamathali za lugha.

Alama iliyotuzwa: **22**

**Kundi la Tatu (Alama 21 – 30)**

Insha katika kitengo hiki huwa inaeleweka vizuri. Hudhihirisha kiasi fulani cha ukomavu wa mawazo. Huwa na mshikamano na mtiririko mzuri kiasi wa mawazo. Insha zinazotuzwa alama **21-25** huwa na ubunifu wa kima cha wastani. Aghalabu watahiniwa hupoteza alama kupitia makosa ya sarufi na hijai, matumizi mabaya ya tamathali za usemi na uakifishaji mbaya. Hata hivyo, mtahiniwa katika kiwango hiki huwa ameikuza mada vizuri.

Insha zinazotuzwa alama **26-30** huwa na ukomavu zaidi wa mawazo. Maudhui hushughulikiwa kikamilifu zaidi na huwasilishwa kwa mtindo unaovutia zaidi. Insha katika kijitengo hiki hutosheleza urefu. Hata hivyo, insha hizi bado huwa na makosa kiasi ya sarufi na hijai.

**Mtungo wa Tano**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

**Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.**

MAJUTO MAKALI

Sikujua kuwa ningejuta majuto ya mjukuu. Kweli, nilijipanza. Nilikuwa na wasena wangu watatu; Matata, Pato na Salim. Tulikuwa marafiki wa dhati, kula kubakishiana, kufa kuzikana. Tulipendana kama chanda na pete. Tungefanya mambo pamoja. Katika pilikapilika zetu tungekuwa pamoja. Waama, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Lakini si mambo yote tungeyafanya yangekuwa ya hulka bulibuli. Sikujua kwamba wananipotosha polepole tu! Siku moja, wasena wangu walisema kuwa tuende tukaibe mihadarati ili tuitumie.

Nilikuwa ninasita sita kukata abadan katan lakini nilivutiwa la kwamba sikuwahi tùmia mihadarati. Nilikuwa safi kama sufi. Sikujua kuwa ninajitia hatarini. Ole wangu!

Ni kama macho yangu yalifunikwa na pazia na kuenda dhidi ya methali, macho hayana pazia. Ningepatwa na masaibu yatakayonisibu. Tulitoka shuleni na kuenda kuiba mihadarati. Bila shaka, hatukupatikana na kuelekea misituni. Tulidhani kuwa mihadarati inafanya akali zako ziwe nyepesi lakini la!

Tuliitumia mihadarati na tukawa tumelewa chopi! Kweli, tulivalia miwani. Tulikuwa samaki na tukatambaa kote msituni. Hatukujua kuwa mwenye mihadarati alituona tukiiba. Tulikuwa katika maisha ya raha mustarehe.

Matopa ya vitabu, tuliyatupa, sare, tuliichoma. Tulitengana na masomo kama ardhi na mbingu. Ghafla bin vuu, insi mmoja alipiga kamsa na kusema, "Ni wale! Washike!" Tuliduwaa na,

kubung'aa. Ilikiwa mwenye mihadarati na maafisa.

Tulisalimu amri na kufungwa

pingu. Wavyele wetu waliitwa. Kweli, niliwafuata wasena wangu kihalela. Nilijiponza kisha kupata madhara. Kweli, niliona cha mtema kuni. Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Mtahiniwa huyu amedhihirisha ukomavu zaidi katika uelewa wa mada. Ameshawishiwa na wendani wake kuiba na kuitumia mihadarati. Mwishowe mtahiniwa huyu anaonyesha athari za kutowazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda. Anatengana na masomo na baadaye kutiwa korokoroni. Mtiririko na mshikamano wa insha hii una upungufu kwa kuwa mtahiniwa huyu ghafla anaeleza walivyotupa matopa ya vitabu na kuchoma sare ya shule. Utungo huu una kosa mantiki kwani mtiririko na mshikamano wa mawazo hujakuzwa vyema. Tunafahamu kuwa biashara ya mihadarati si halali. Mbona polisi na mwenye mihadarati waandamane? Polisi wangemtia baroni.
Baadhi ya makosa aliyotenda ni:

a) Tuende badala ya twende
b) Nina sita sita badala ya ninasitasita
c) Kukata abadan katan badala ya kukataa abadan katan
d) Kuenda badala ya kwenda
e) Akali zako badala ya akili zetu.
f) Hatukupatikana na kuelekea msituni ingekuwa hawakutupata kwani tulielekea msituni.
g) Tulikuwa katika maisha ya raha mustarehe badala ya tulikuwa katika hali ya furaha...

Mtahiniwa huyu hata hivyo alizingatia vipengele vifuatavyo;

a) Amekuza mada ifaavyo.
b) Amepangilia kazi kiaya.
c) Amewaumba wahusika waliomponza.
d) Ametumia msamiati kwa njia bora. Aidha ametumia tamathali za usemi kuleta mnato kwa mfano tashbihi, tulipendana kama chanda na pete, kutengana na masomo kama ardhi na mbingu, methali kwa mfano umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, misemo kama vile macho hayana pazia na tulivalia miwani.

Alama iliyotuzwa: **28**

**Kundi la Nne (Alama 31 – 40)**

Watahiniwa katika kundi hili kwa kawaida huwa wanaimudu lugha vizuri. Huwa na kiwango cha juu cha ubunifu kimaudhui na kifani. Hutumia lugha kwa wepesi kujieleza. Mijadala au masimulizi yao huwa na muundo bayana wenye mshikamano na mtiririko mzuri wa mawazo. Hawa huielewa mada na kuikuza kwa kiasi cha kuridhisha. Wale wanaotuzwa alama **31 - 35** huitumia lugha kwa wepesi zaidi. Hata hivyo, insha zao huwa na makosa ya hapa na pale ya sarufi, hijai na msamiati.

Wale wanaotuzwa alama **36 - 40** huwa na umilisi wa lugha wa kiwango cha juu zaidi na huwasilisha mawazo yao kwa mitindo mbalimbali ya usimulizi ambayo huzipa kazi zao mvuto wa hali ya juu. Huteua msamiati unaoafiki mada na kuutumia vyema kufanikisha usimulizi au mjadala wao. Insha zao huwa na makosa machache mno ya sarufi, hijai na msamiati. Hali kadhalika hati zao zinasomeka kwa urahisi na wanatosheleza urefu.

**Mtungo wa Sita**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

**Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu ~~kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda~~**

JITAHADHARI KABLA YA HATARI

Nilikuwa pale gerezani huku machozi yakinipukutika kupukupu na kuzilovya nguo zangu chepechepe. Nilijawa na uchungu moyoni huku nikielewa fikra kuwa mwiba wa kujidunga hauambiwi pole. Nilitamani niyarudie maisha yangu ya ujana lakini lo! Ujana ni kama moshi ukienda haurudi. Niliyakumbua maisha yangu ya awali na kukumbuka jinsi yalivyokuwa yamekumbwa na matatizo.

Wazazi wangu-Bi na Bwana Walalahoi- walikuwa maskini hadi maskini wenzao waliwacheka na kuwaita maskini. Nilizaliwa kama mtoto wa pekee. Hata hivyo, maisha hayakuwa ya kula paipai kwa kijiko. Shuleni, nilienda huku sare zangu zikiwa na vipaka vya kila aina. Kwa umbali, ungedhani ni rangi za upinde. Shuleni,

sikuwa kipaumbele wala anayeshika mkia. Hata hivyo, nilijifunga kibwebwe huku nikielewa kuwa limu ni johari.

Nilipokuwa nikirejea nyumbani baada ya kufukuzwa kutokana na kutolipa karo, nilipashwa ujumbe kuwa wazazi wangu walikuwa wameabiri merikebu ya jongomeo baada ya kuhusika katika ajali isiyojali. Nilipigwa na mughma kupitia kiasi. Wingu la simanzi lilitandaa angani kote. Woga wa kunguru ukanivamia. Je, ni nani angenilipia karo na kunikabidhi mahitaji yangu? Sikuweza kufikiria maisha bila wazazi wangu.

Baada ya mazishi, wengi waliniahidi kuwa wangenikabidhia mahitaji yangu. Lakini niliamini kuwa maneno hayo yalikuwa ya kusema tu. Mali waliokuwa nazo wazazi wangu zilichukuliwa kwa kuwa walikuwa wakiwadai watu wengi. Amakweli, Ibilisi wa mtu ni mtu.

Sikuwa na budi ili kujiunga na marafiki wenzangu wenye tabia benibeni ili kupata mahitaji ya kila siku. Si jambo la kustaajabisha kuwa baada ya muda wa kidinya, nilipotoka maadili na kujitoma katika ulimwengu wa anasa. Nao ukanipokea kwa mikono miwili na kunichezea ngoma nitakazo.

Gange ya kila siku ikawa kuichana mitaa kama mbwakoko na kuwapokonya watu mali. Wahenga na wahenguzi hawakukosea waliponena kuwa

siku za mwizi ni arubaini. Siku moja tulipokuwa katika mchochoro ule tukiwangoja wateja, tulikutana ana kwa ana na maafisa wa polisi. Wenzangu walitundika miguu begani na kuniacha pale huku nikiwa nimevaa miwani. Nilipokea kichapo mithili ya mbwa aliyetabawali msikitini. Niliporudisha fahamu, nilikuwa pale korokoroni huku nikiwa nimefungwa vikuku mkononi. Machozi ya majonzi yalinitiririka tiriri. Nikaelewa fika kuwa majuto ni mjukuu huja baadaye.

Baada ya siku tatu, nilipelekwa mahakamani ili kesi isikilizwe. Baadaye, hakimu alitoa hukumu kuwa ningekula kalenda kwa miaka ishirini kutokana na kusumbua imani ya wanakijiji. Hakika, nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuikuza kwa mtindo mpevu zaidi akilinganishwa na wa awali. Ametumia mbinu rejeshi kuelezea hali iliyomkumba baada ya kupoteza wazazi wake kutokana na ajali ya barabarani. Ametumia vipengele mbalimbali vya kimuundo na kimtindo kuipamba insha yake kama vile :

a) **Methali-** ujana ni moshi, ukienda haurudi na siku za mwizi ni arobaini.
b) **Sitiari-** Kuabiri merikebu ya jongomeo kwa maana ya kuaga dunia.
c) **Nahau-** kupigwa na mughuma, kuvaa miwani na kula kalenda.
d) **Maswali ya balagha-** je, ni nani angenilipia karo na kunikidhia mahitaji yangu?
e) **Tashbihi-** Kuichana mitaa kama mbwakoko.
f) **Tanakali za sauti-** Majonzi yalinitiririka tiriri.

Mtahiniwa huyu ana hati nadhifu na amepangilia mawazo yake kiaya. Urefu wa insha yake umejitosheleza. Utungo huu una makosa machache kama vile :

a) Shuleni sikuwa kipaumbele badala shuleni sikuwa nikiongoza masomoni.
b) Wingu la simanzi lilitandaa angani badala ya lilitanda angani.
c) Kunikabidhi mahitaji yangu ? ingekuwa kunikidhia mahitaji yangu.
d) Mali waliokuwa nazo badala ya mali waliokuwa nayo. (Kosa la ngeli)

Kwa jumla, insha hii imebainisha uasilia wa hali ya juu, ina mvuto mkuu kutokana na namna mtahiniwa alivyotumia lugha kwa ustadi.

Alama iliyotuzwa: **34**

## Mtungo wa Saba

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

*Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:*

Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Kila nionapo wasichana wa rika yangu wakifululiza hadi shuleni, wingu la simanzi hutanda tuadini mwangu. Machozi ya majonzi huniminika bwaibwai kama ngamia mkongwe aliyejipata kichinjioni. Najiuma kidole kwa kuwa beramu ambayo daima dawamu hufuata upepo. Nalilia ujana wangu lakini ni bure bilashi. Yalikuwa tayari yamemwagika. Yasingezoleka.

Ilikuwa msimu wa choka nilipojiunga na shule ya upili ya Sime Masomoni. Baada ya kufuzu katika mtihani wa kitaifa, nilikuwa nimesajiliwa katika shule hiyo ya kutiliwa ngoa kote nchini. Hata hivyo, ingekuwa muhali kubuka nambari wahedi kwani sime nyingine masomoni zilikuwa zikichuania nambari hiyo. Katika mtihani wa kwanza, nilipata alama za ibra na shani. Nilikuwa nimeberaza mgwisho darasani mwangu. Hali hii ya kuvuta mkia darasani ikawa sheria japo nilijitahidi mno.

Hivyo basi, ili kujisetiri fedheha yangu ya mgoni, nilijiunga na kundi la wasichana watundu. Kundi hilo lilijulikana kote, mote na pote kwa ukaidi wao wa mkia wa nguruwe. Hata hivyo,

nilijiunga nao huku nikimaizi kuwa heri nusu shari kuliko shari....

Kundi lile lilinilaki kwa moyo mkunjufu nami nikadhani kuwa walinipenda kama pumzi za uhai. Kwa mwendo wa kobe, nilianza kuwapenda na kutangamana nao zaidi. Laiti ningalijua mumbi nilikuwa nimejilisha.

Baada ya siku ayami, walianza kunirai nitumie mihadarati. Awali nilikataa katakata lakini, baada ya kunisihi mara anuwai, nilisalimu amri na kukubali; shingo mkingamo. Nilipojaribu sigara ilinichafua moyo. Hata hivyo, ulamaa wenye busara na tabasuri hakudata dango walipodhukuru, mtu akichovya hachovi mara moja. Hulka na silika hiyo ilianza kuniandama kama mtu na kivuli chake. Nikawa mraibu sugu na sagamba wa dawa za kulevya. Hata hivyo, hazikukidhi matakwa yangu ya uraibu. Nikajaribu, si kokeni, si heroini, si bangi, si miraa, yakini si yamkini, kitumbua changu kilikuwa kimeingia mchangani.

Kutia chumvi kwenye bangusi, nilipowaona wakichanganya miguu hadi vilabuni, sikuchelewa wala kukawia kuwafuata. Sikutaka kuwa yule mtu pweke ambaye ni uvundo. Huko kilabuni, kulikuwa na tembo ya maazi. Nilipoisharabu nilingiwa na hamu,

hamumu na uchu wa kuisharabu tena. Waama, tindi moja, tindi mbili, tindi tatu mazoea.

Isitoshe, wazee waliokuwa wamekula munyu walibanana humo kama kuni uchagoni. Japo 'marafiki' yangu waliniambia nijaribu ngono na wazee hao, nilikataa. La hasha! Singefanya ngono na bwana wa mtu; alaa, kulihali.

Siku moja, nilipokuwa nimeenda kilabuni, niliagizia tembo. Nikanywa kwa bashasha mpwitompwito pasi na kujua dawa za ganzi zilizokuwa zimewekwa kwenye kinywaji changu. Kwa muwia wa kelbu kukalia mkia wake, nilipoteza fahamu. Usiku ukawa mrefu na vitendo visivyoandikika.

Nilipopata fahamu, nilikuwa katika ambulensi huku ngeu imelowesha lebasi zangu chepechepe. Punde si punde, tulimwasili kwenye zahanati ya Pole Sana. Kundi la matabibu lilinitia kwenye machela na kunifikisha kwenye wodi. Likanidunga sindano ya ganzi nami nikazimia. Nilipopata fahamu, niliwapata wavyele wangu wakiwa katika huzuni. Tabibu mmoja akakuja ... kutuarifu kuwa nilikuwa na virusi vya UKIMWI, licha ya kuwa mjamzito.

Hakika nilikuja kugundua kwamba ni muhimu kuwazia hatari ya kufuata yale ambayo marafiki wanatenda.

Mtahiniwa huyu amelenga ndipo. Amekuza maudhui kwa kutumia lugha vyema. Tofauti na watangulizi wake, mtahiniwa huyu amekikuza kisa kinachoibua hisia nzito kwani baada ya kushawishiwa na marafiki wake kushiriki ulevi baadaye anatiliwa dawa zinazomfanya mtu kusinzia (za gonezi) kwenye kileo. Yaliyomfika ni mambo ya kutamausha kwani aliambulia uja uzito na virusi vya Ukimwi.

Mtahiniwa huyu ametumia vipengele anuwai vya kimuundo na kimtindo kama vile;

a) Kujenga taharuki katika aya ya kwanza. Hatujui mbona wingu la simanzi hutanda fuadini (moyoni) mwake kila awaonapo wasichana wa rika lake. Mbona anajiuma kidole kwa kuwa beramu?
b) Mdokezo wa methali- yalikuwa yamemwagika. Yasingezoleka.
c) Nahau- Kusalimu amri.
d) Tashbihi- Hulka na silka kumwandama kama mtu na kivuli chake.
e) Tabaini- Nikajaribu si kokeni, si heroini, si bangi, si miraa, yakini si yamkini.

Isitoshe, mtahiniwa huyu ametumia visawe vya misamiati mbalimbali kuondoa ukinaifu. Kwa mfano : Ametumia :

- Kelbu badala ya mbwa
- Ngeu badala ya damu
- Lebasi badala ya nguo
- Fuadini badala ya moyoni
- Beramu badala ya bendera
- Gonezi badala ya usingizi

Kadhalika, ameteua lugha ambayo inajenga taswira anuwai za hali ambayo anasimulia. Insha ya mtahiniwa huyu ina mshikamano na muwala wenye mantiki kutoka mwanzo hadi mwisho. Msomaji anajipata akisoma ili kung'amua yatakayojiri.

Makosa machache yamejitokeza ni kama vile :

a) Rika yangu badala ya rika langu. Rika ni nomino katika ngeli ya Li-Ya.
b) Nilikuwa nimesajiliwa badala ya nilisajiliwa.
c) Marafiki yangu- marafiki wangu.
d) Methali heri nusu shari kuliko shari... haichukuani na kauli tangulizi.

Kwa jumla hii ni insha ambayo inabainisha uasilia na ubunifu asilia wa mtahiniwa wa kiwango hiki.

Alama iliyotuzwa: **37**

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

Ni dhahiri kwamba japo alama wastani katika Lugha imedidimia, utendaji wa wanafunzi katika Insha unaendelea kuimarika kinyume na hali ilivyokuwa mwaka wa 2018. Ili kuimarisha umilisi wa wanafunzi katika Ubunifu na Mawasiliano, yafuatayo yanapendekezwa:

4.3.1 Walimu wawahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi katika mada tata za sarufi.

4.3.2 Ufunzaji wa msamiati uhusishwe na muktadha badala ya kuufunza ukiwa mkavu. Kwa mfano, msamiati wa mazingira unaweza kufunzwa kwa kutumia ufahamu kuhusu mazingira. Hili litamwezesha mwanafunzi kuuelewa msamiati katika matumizi halisi.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kutumia ujuzi wa waliyosoma katika ufahamu kujibu maswali ya ufahamu badala ya kukariri au kuchopoa mawazo moja kwa moja kutoka kwenye vifungu.

4.3.4 Wanafunzi wahimizwe kutumia mbinu bora za kuukabili ufahamu. Badala ya kusoma swali, kisha kuanza kutafuta majibu, wasome ufahamu kwanza kabla ya kuyasoma maswali na majibu yaliyotolewa. Aidha watambue vidokezo muhimu katika kila aya.

4.3.5 Walimu watunge maswali yanayopima stadi mbalimbali (ngazi/viwango) tofautitofauti za maarifa au utambuzi wala si stadi ya kukariri/ujuzi pekee. Hili litamzoesha mwanafunzi kujibu maswali ya aina tofautitofauti katika mtihani.

4.3.6 Stadi ya kusikiliza na kuzungumza ihimizwe zaidi kupitia utambaji, mijadala na imla, kusikiza vipindi vya redio na vipindi vilivyorekodiwa ili kuboresha maendelezo na kuimarisha mitindo ya kujieleza au mitindo ya usimulizi.

4.3.7 Wanafunzi wasisitiziwe umuhimu wa kusoma vitabu na makala mbalimbali ili kukuza ubunifu.

4.3.8 Wanafunzi waelekezwe kuhusu uteuzi ufaao wa vipengele vya kimtindo huku wakishauriwa dhidi ya kushinikiza msamiati usiohitajika katika insha. Hili hufifilisha mawasiliano na kuifisidi insha mvuto wake. Msamiati unaoteuliwa sharti uoane na mada na kuafikiana na msamiati au matini jirani katika sentensi ambamo umetumiwa. Msamiati wa kishairi usitumiwe kuandika tungo zisizo za kishairi.

4.3.9 Walimu na wanafunzi warejelee vitabu mbalimbali vilivyopendekezwa na kuidhinishwa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala. Wasitumie kimoja tu. Hili litawapa wanafunzi uwanja mpana wa kujifunzia.

4.3.10 Walimu wawasisitizie wanafunzi umuhimu wa hati nzuri ili kurahisisha usomaji na usahihishaji wa insha zao na kuzipa kazi zao mvuto chanya.

4.3.11 Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ili kuimarisha mikakati ya kujieleza na kusimulia kwa kwacho.

4.3.12 Walimu wawaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufasiri mada/maswali mbalimbali ili kukinga dhidi ya kupotoka kimaudhui.

4.3.13 Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya mitindo tofautitofauti ya insha ili wapate uzoefu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

4.3.14 Walimu watumie mwelekeo mseto katika ufunzaji wa mada mbalimbali, kwa mfano mada changamano za kisarufi. Mathalan, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya hadithi kufunzia dhana za kisarufi kama vile njeo, hali na aina za maneno. Hili litakinga dhidi ya wanafunzi kuziona dhana hizi kuwa dhahania. Itakuwa rahisi kuzielewa dhana hizi zikitokea katika matumizi halisi. Kadhalika hili litayafanya mafunzo ya sarufi kuwa ya kuvutia zaidi, hivyo wanafunzi watayachangamkia na kuyaelewa zaidi.

4.3.15 Waalimu wawaongoze wanafunzi kufanya vikundi vya kujadili na kufanya mazoezi kuhusu mada mbalimbali zilizofunzwa. Hili litawaweza wanafunzi kufaana wao wenyewe.

4.3.16 Ikiwezekana shule jirani zinaweza kufanya warsha na kongamano kujadili masuala mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

4.3.17 Waalimu vilevile wapange ziara za kutembelea Taasisi mbalimbali zinazokuza lugha ya Kiswahili ili kupanua maarifa ya wanafunzi. Taasisi hizo ni kwa mfano Idhaa za utangazaji, Matbaa, Taasisi ya Ukuzaji Mitaala na hata Idara ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini.

4.3.18 Wanafunzi wahimizwe kushiriki katika Tamasha za Muziki na mashindano yoyote yanayolenga kukuza Lugha kwa ujumla kwa mfano Drama.